MWONGOZO – LUCHA – KIBAADA MWIGO
1

1. **UFAHAMU**

a) **Onyesha dhuluma nne dhidi ya jinsia ya kike katika jamii kwa mujibu wa kifungu hiki.** **(alama 4)**

i. Kuondolewa shuleni / kukatisha masomo.
ii. Msichana anapopata mimba hukataliwa na wazazi.
iii. Wanaume kuwadandia wasichana wadogo na kuwabaka.
iv. Kuambukizwa magonjwa ya zinaaa.
v. Kupachikwa mimba. Za kwanza 4x1=4

b) **Bainisha hali zinazoweza kulaumiwa kwa changamoto zinazowakumba vijana wasichana.** **(alama 5)**

i. Matumizi ya mihadarati / dawa za kulevya.
ii. Umaskini.
iii. Wanaume wenye ashiki.
iv. Mahitaji ya kifamilia.
v. Ukosefu wa malezi bora au ushauri au mafunzo kutoka kwa wakubwa.
vi. Kugeuza ngono kuwa bidhaa ya kibiashara.
vii. Ureda
viii. Porojo na hekaya za marika zao, majarida ya kutilika shaka, wavuti na sinema zisizoaminika kuhusu ngono. Zozote 5x1=5

c) **Eleza tofauti kati ya maisha ya zamani na maisha ya kisasa.** **(alama 3)**

i. Wasichana zamani walipata mimba kinadra lakini sasa mimba kwa wasichana wadogo ni jambo la kawaida.
ii. Zamani maadili yalizingatiwa sana lakini sasa yamedidimia.
iii. Zamani kina nyanya na babu walitoa mafunzo ya utuuzima kwa wajukuu jambo ambalo halipo nyakati za sasa. Zozote 3x1=3

d) **Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kifunguni.** **(alama 3)**

**i.** Tukizi – nadra / muhali / ilikuwa ngumu
**ii.** Harara – hisia / mshawasha / nishai / tamaa/ shauku
**iii.** kupata himila – kuwa waja wazito / kupata mimba. 3x1=3

Toza ½ alama kwa kila kosa la sarufi linapotokea mara ya kwanza hadi makosa sita.
Sarufi ½ hadi sita- alama 3
Hijai ½ hadi sita – alama 3

2. **UFUPISHO (Alama 15)**

a) **Dondoa mambo muhimu yanayojitokeza katika aya za kwanza tatu. (maneno 80 - 90)** **(alama 10, utiririko 1)**

- Juhudi za kushughulikia changamoto za usalama zimeimarishwa kwa matumizi ya teknolojia.
- Huduma zinazotolewa na polisi kwa umma zimewafikia kwa njia rahisi.
- Maendeleo ya kiteknolojia yamehusishwa na hatari fulani.
- Matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuukabili uhalifu wa jinai si suala geni.
- Kuimarika kwa ubunifu wa wahalifu.

- Vikosi vya usalama vinafaa kujipiga msasa zaidi ili kuzuia au kuzima kabisa njama za kihalifu.
- Matumizi ya teknolojia katika kuzuia visa vya uhalifu yameanza kukubalika na wanajamii.
- Vifaa vya kuchunguza iwapo mtu ana kifaa chochote cha chuma vimezuia pakubwa uhalifu wa utekaji nyara.
- Vifaa vya kudhibiti kasi ya magari vimeimarisha usalama barabarani.
- Uwekaji wa taa za umeme kwenye viunga vya miji huuhakikishia umma usalama wao na kuwafichua wavamizi
- Kamera za siri ni muhimu wakati wa kesi zinazohusisha uvamizi au uhalifu.
- Vifaa vidogo vinavyotumia mawimbi ya kielektroniki ni muhimu wakati wa mawasiliano ya dharura.
- Wazee ni windo jepesi la wahalifu.
- Kuna teknolojia inayotumia miale kufichua silaha haramu au kumtambua mihadarati.

(Yaliyomo-hoja 9 x 1 = 9)
Mtiririko=1

**b) Ukirejelea aya tatu za mwisho, onyesha changamoto za teknolojia ya kisasa kwa maneno 45 - 50.** **(alama 5, utiririko 1)**

- Vifaa vya kwenda kasi kuwafuata wahalifu huhatarisha mtumiaji, mshukiwa na raia.
- Kifaa cha kuzima kasi ya magari kwa mbali kinaweza kulisimamisha gari ghafla na kusababisha maafa makubwa.
- Matumizi ya mwangaza mkali au gesi kumdhibiti mhalifu husababisha ulemavu wa kuona na kupumua.
- Vifaa vinavyotumia miale huwa na athari ya kudumu na kusababisha maradhi ya kansa.

Yaliyomo - hoja 4 x 1 = 4
Mtiririko= 1
(Alama= 5)

SARUFI = **6 x $^1/_2$=3)**
HIJAI **6 x $^1/_2$=3)**

3. **MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**i – i – twa - yo**

a) alama 1/0

b)

i. Sauti mviringo /u/
ii. Sauti mwambatano /ngw/ 2 × ½ = 1

c) Neto alimzolesha Salim takataka nyingi. alama 2/0

d) Mvulana aliwasha moto kisha akaukunjua mkeka. alama 2/0

e) Wanyama: ndovu / tembo, "rhino" na ngiri (wanyama wa pori wote) hupatikana katika Mbuga ya Maasai Mara. AU

Wanyama --- ndovu / tembo, *rhino* na ngiri (wanyama wa pori wote) hupatikana katika Mbuga ya Maasai Mara. 8 × ½ = 4

f) Mbuzi wa majirani zangu waliibwa na akina mama hao. alama 2/0

g)

<table>
<tr><td colspan="7">S</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="3">S1</td><td>U</td><td colspan="3">S2</td><td>1</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="2">KT</td><td></td><td>KN</td><td colspan="2">KT</td><td>1</td></tr>
<tr><td>N</td><td>Ts</td><td>T</td><td></td><td>N</td><td>T</td><td>E</td><td>2</td></tr>
<tr><td>Mwizi</td><td>alijaribu</td><td>kulitetea</td><td>lakini</td><td>umati</td><td>haukumwamini</td><td>kabisa</td><td>1</td></tr>
</table>

h) Mbwa yule alibweka bwe! alama 1/0

i) Yaliyoliwa alama 3/0

j)
   i. Wa 'lakini
   ii. Nisaidi 'e 2 × 1 = 2

k) Tulibeba maji ya kutosha – kishazi huru
tulipoenda Tomoko – kishazi tegemezi 2 × 1 = 2

**l) Kiambishi 'm'**

i. Nafsi ya pili wingi: **m**takuja?
ii. Nafsi ya tatu umoja: ali**m**letea
iii. Umbo la nomino za ngeli ya A- WA umoja: ***m**tu – watu, **m**ja – waja.*
iv. Umbo la nomino za ngeli ya U- I umoja: ***m**kate – mikate, **m**kono – mikono.*
v. Konyesha mahali ndani: *mahali **m**le **m**na siafu.*
vi. Kuonyesha weledi wa mtu / kuonyesha nomino / unominishaji: ***m**pishi, **m**shoni, **m**somi.* (3 × 1 = 3, matumizi = ½ , mfano = ½ )

m) Uzuri – nomino ya pekee / maalum / mahsusi
Aila - nomino ya jamii / makundi 2 × 1 = 2

n) Nyumba nzuri itajengwa hadi kesho. alama 2/0

o) Mwerevu huumia mjinga akierevuka. alama 2/0

p) Panda mtini uangue matunda – kuugiza / kuelekeza / sentensi agizi / elekezi.
Yameiva vizuri – kutaarifu / kutoa ujumbe/ sentensi ya taarifa. 2 × 1 = 2

q) Kunyweni! / mnyweni! alama 1/0

r) U – ZI / ZI alama 1/0

s) Pata jiko / asi ukapera alama 1/0

t) Chovya chovya, humaliza buyu la asli. alama 1/0

SARUFI = ITEGEMEE ALAMA KWA SWALI HIJAI **6 x $^1/_2$=3)**

4. **ISIMUJAMII**

**a)**

- Kutumia lugha inayoeleweka/nyepesi/sahili/ya kufafanua. "Hamna faida yoyote ya kujiua."
- Kutumia maswali ya balagha ili kumshirikisha na kuvuta makini yake. "Ukijitoa uhai utanufaikaje?"
- Kutumia lugha ya mvuto/kushawishi/'Beste yangu fikiria maisha sio kifo.'
- Kutumia lugha ya ucheshi 'Msee ukijimurder utanufaikaje sasa?'
- Kuchanganya au kubadili msimbo /lugha ili kusisitiza ujumbe na kurahisisha kuelewa. "Kwani ukicommit suicide utanufaikaje?"
- Kutumia viziada lugha/ ishara za uso, mikono, miondoko ya mwili ili kusisitiza hoja.
- Kutumia lugha ya kuelekeza/kushauri. "Maisha yako yana manufaa kuliko kifo."
- Kutumia chuku. "Ukijitoa uhai utaenda kwa shetani direct."
- Matumizi ya msamiati teule 'uhai,maisha,suicide,msongo wa akili, Mungu,Yesu Kristo.'
- Kutumia tasfida inapohitajika badala ya kutumia kauli kama kujiua unasema "kujitoa uhai."
- Matumizi ya lugha sanifu "Tafadhali fikiria tena maisha yako."
- Matumizi ya masimulizi ya visa vya watu waliofikiria kujitoa uhai lakini wakabadili nia.
- Matumizi ya nyimbo/wimbo wa kumshinikiza asijiue.
- Kutumia toni /kiimbo cha ukali/ kuonya inapohitajika .
- Matumizi ya mbinu ya maombi/sala.
- Matumizi ya lugha legevu/isiyo sanifu. "msee, tumaisha uhitaji ujasiri: Punguza stress."
- Matumizi ya mbinu ya majibizano / kudadisi "Kwani ni yapi umepitia ukafikiria hivyo?"
- Kutumia sentesi /kauli fupi. "Beste yangu chagua maisha." **Za kwanza 6 x 1 = 6)**

**Tanbihi - mifano itolewe ili alama kamili itolewe.**

**b) muktadha**

i. mzungumzaji huchota msamiati kutoka mahali anapozungumzia. Mfano: atatumia msamiati wa sokoni akiwa sokoni, lugha ya mahakamani akiwa mahakamani.

ii. Muktadha huathiri kiimbo. Mfano, mtu akiwa darasani huzungumzia kwa kiimbo cha chini.

iii. Muktadha huathiri uteuzi wa msimbo / lugha / lahaja ambayo mtu anatumia. Mfano, muktadha rasmi humtaka mtu kutumia lugha rasmi kama Kiswahili na Kiingereza.

iv. Muktadha hudhibiti kiwango cha usanifu na urasmi wa lugha. Mfano, muktadha usiyo rasmi hayahitaji kutumia lugha yenye usanifu na urasmi, mtu anaweza kutumia hata simo / misimu.

v. Muktadha hudhibiti ishara anazotumia mtu. Zipo ishara nyingine na miondoko ambayo haikubaliki / ni mwiko katika baadhi ya muktdha / tamaduni.

vi. Muktadha hudhibiti mtindo nafsi wa mtu. Kwa mfano, mtu katika mnada au biashara ya rejareja huweza kujirudiarudia ili kuwavutia wateja. **Za kwanza 4 x 1 = 4**

SARUFI = **4 x $^{1}/_{2}$=2)**

HIJAI **4 x $^{1}/_{2}$=2)**